# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA APRILI, 2019 NA MWELEKEO WA MEI, 2019

**Dondoo za Aprili, 2019**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya viashiria pamoja na mwenendo wa mvua kwa mwezi Aprili, 2019 na mwelekeo wa viashiria na matarajio ya mvua kwa mwezi Mei, 2019 nchini.

a) Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2019 maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka yalipata vipindi vichache vya mvua hususan katika wiki ya kwanza ya mwezi. Aidha, uwepo wa kimbunga *KENNETH* ulisababisha ongezeko la mvua katika wiki ya mwisho ya mwezi hususan katika maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria, magharibi pamoja na ukanda wa pwani. Hata hivyo, mtawanyiko wa mvua katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki umeendelea kuwa hafifu.

b) Maeneo mengi ya nchi yanayopata mvua mara moja kwa mwaka yameendelea kupata mvua za '*Msimu*' zikiendelea kupungua taratibu kuelekea mwisho wa msimu kama ilivyotarajiwa, na mtawanyiko katika maeneo mengi umekuwa wa kuridhisha, isipokuwa katika maeneo machache ya kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida).

## 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI APRILI, 2019.

Mvua za Masika zimeendelea kunyesha vizuri katika mwezi Aprili, 2019 kwa baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (pwani ya kaskazini na kanda ya ziwa Victoria), hata hivyo, mtawanyiko wa mvua umekuwa hafifu katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Kutokea kwa kimbunga *Kenneth* katika bahari ya Hindi kuelekea rasi ya Msumbiji (Magharibi mwa Madagascar) kumesababisha ongezeko la mvua katika maeneo mengi ya nchi hususan wiki ya mwisho ya mwezi Aprili, 2019. Maeneo mengi ya nchi yanayopata mvua mara moja kwa mwaka yameendelea kupata mvua za '*Msimu*' kama ilivyotarajiwa katika kipindi cha mwezi Aprili, 2019 pia uwepo wa kimbunga Kenneth uliweza sababisha kuwepo kwa vipindi vya mvua kubwa katika baadhi ya maeneo hapa nchini.

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI MEI, 2019

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la bahari la juu ya wastani inatarajiwa katika eneo la Kitropiki la Bahari ya Pasifiki, mashariki mwa Bahari ya Hindi pamoja na maeneo ya kati Kusini mwa Bahari ya Hindi. Hali kadhalika, joto la wastani hadi chini kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantic karibu na pwani ya Angola. Hali ya joto la chini kidogo ya wastani inayotarajiwa katika pwani ya Angola inatarajiwa kuongeza msukumo wa unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo.

### 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MEI, 2019

Ongezeko la vipindi vya mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya nchi hususan wiki ya kwanza hadi ya pili ya mwezi Mei, 2019 ikifuatiwa na upungufu wa vipindi vya mvua katika wiki za mwisho za mwezi Mei, 2019.

#### 2.2.1 Maeneo Yanayopata Misimu Miwili ya Mvua kwa Mwaka

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo kwa wiki mbili za mwanzo wa mwezi Mei, ikifuatiwa na vipindi vikavu kwa ujumla hususan maeneo ya mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es salaam na kaskazini mwa mkoa wa Morogoro. Aidha, maeneo ya visiwa vya Unguja na Pemba, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa kuendelea.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):** Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache kwa wiki mbili za mwanzo wa mwezi Mei, ikifuatiwa na vipindi vikavu kwa ujumla.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan katika wiki mbili za mwanzo wa mwezi, ikifuatiwa na vipindi vya ukavu.

#### 2.2.2 Maeneo Yanayopata Msimu Mmoja wa Mvua kwa Mwaka

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Vipindi kadhaa vya mvua vinatarajiwa katika wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2019, ikifuatiwa na vipindi vya ukavu.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Vipindi vya ukavu kwa ujumla vinatarajiwa katika kipindi cha mwezi Mei, 2019.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe na kusini mwa mkoa wa Morogoro):** Vipindi vya ukavu vinatarajiwa katika maeneo mengi katika kipindi cha mwezi Mei, 2019 isipokuwa kwa maeneo machache ya kusini mwa mkoa wa Morogoro (Mahenge) ambapo vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa hususan katika wiki mbili za mwanzo wa mwezi Mei.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika ya baadhi ya maeneo hususan wiki mbili za mwanzo wa mwezi Mei, 2019, ikifuatiwa na vipindi vya ukavu kwa ujumla.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):** Vipindi vya ukavu kwa ujumla vinatarajiwa katika kipindi cha mwezi Mei, 2019.

## 2.2 MATARAJIO KWA MWEZI JUNI, 2019

Kwa ujumla kwa kipindi cha mwezi Juni, 2019 hali ya ukavu itakayoambana na vipindi vya baridi inatarajiwa katika maeneo mengi nchini.

## ANGALIZO

Wataalam wakiwemo maafisa ugani katika sekta mbalimbali za uchumi ikiwemo kilimo wafuatilie na kupata taarifa za utabiri wa kila siku na siku kumi kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania na kuwashauri wananchi ipasavyo ili kutumia vyema mvua zinazotarajiwa kuendelea kunyesha katika mwezi huu wa Mei.

Imetolewa na;
**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**